

HOTUBA YA MGENI RASMI KATIKA KILELE CHA MAADHIMISHO YA SIKU YA WANAWAKE DUNIANI INAYOFANYIKA KIWILAYA KATIKA KATA YA IGOMA KIJJI CHA IGOMA HALMASHAURI YA WILAYA YA MBEYA TAREHE 08.03.2017

Mheshimiwa Mwenyeviti mwenyeji wa Kijiji cha Igoma
Waheshimiwa Madiwani wa Halmashauri ya wilaya
Waheshimiwa wenyeji wa vijiji vyote vya kata ya Igoma na kata jirani
Waheshimiwa viongozi wa chama Tawala
Waheshimiwa Viongozi wa vyama mbalimbali vya kisiasa
Waheshimiwa viongozi wa Dini na Asasi zisizo za kiserikali
Ndugu, Mkurugenzi wa Halmashauri za Wilaya ya Mbeya
Wakuu wa Idara na Vitengo
Wanavikundi wote wa Halmashauri ya wilaya ya Mbeya
Wananchi wote waalikwa mabibi na mabwana

Awali ya yote nachukua fursa hii kumshukuru mwenyezi Mungu kwa kutuweka hai hadi siku hii ya leo. Pia natoa shukrani zangu za dhati kwa uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kwa kuniteua kuwa Mgeni rasmi kwenye kilele cha maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani mwaka huu 2017. Vilevile natoa shukrani za dhati kwa maandalizi mazuri yaliyofanyika katika kufanikisha maadhimisho haya ambayo Kiwilaya yanafanyika katika kata ya Igoma kijiji cha Igoma.

Ndugu wananchi,

Pamoja na jitihada zote zilizofanyika za kuratibu shughuli hii, kama washiriki wa siku hii msingetikia wito, basi juhudi zote zingepotea bure, hivyo nachukua fursa hii kuwashukuru wote kwa kufika kwenu na ninawakaribishe sana katika maadhimisho ya siku ya wanawake Duniani.

Ndugu Wananchi,

Nimefarijika sana kusikia wadau mbalimbali, asasi za kiraia na wanajamii kwa ujumla wamejumuika katika kufanikisha sherehe za maadhimisho ya siku ya wanawake duniani. Natumia fursa hii kusema asanteni sana pia kuwatia nguvu kuendelea na moyo huo wa kujitoa katika shughuli kama hizi katika jamii yetu.

Ndugu wananchi,

Kauli mbiu ya Maadhimisho ya Siku ya wanawake duniani kwa mwaka 2017 inasema

“TANZANIA YA VIWANDA, WANAWAKE NI MSINGI WA MABADILIKO YA KIUCHUMI” kauli mbiu hii inalenga kutoa ujumbe ufuatao kwa jamii ya Watanzania:

- Kuwawezesha wanawake kushiriki kikamilifu na kwa ufanisi katika kutambua uwezo wao wa kubaini kutumia rasilimali zilizopo ili kujiongezea kipato na kuondoa umasikini na hivyo kijiletea maisha bora zaidi.

- Kuwawezesha wanawake kuingia katika uchumi wa viwanda vidogo vidogo na kuweza kujiajiri na kuajiri wengine.
- Kuiwezesha jamii ya watanzania kuuona bayana na kuupa thamani inayostahili mchango wa wanawake katika maendeleo yao ya familia zao na ya Taifa kwa ujumla, jamii kupanga na kutekeleza mipango itakayozingatia usawa wa kijinsia.
- Kuwawezesha wanawake ambao walio wengi ni wazalishaji mali katika sekta ya kilimo, ufugaji na uvuvi, uchimbaji madini, viwanda vidogo vidogo na ujenzi. Wanawake katika sekta ya kilimo wanakabiliwa na tatizo la nyenzo duni, ukosefu wa mitaji, ujuzi mdogo, na kutokuwa na milki ya ardhi.
- Kuelimisha jamii kutambua na kuisitiza kuwa usawa wa kijinsia unapatikana tu kutakapokuwa na mizizi thabiti ndani ya familia na kaya za jamii za watanzania.
- Kuwawezesha wanawake kuwa na mazingira mazuri ya kisheria yatakayohakikisha kuwa hapatakuwepo na sheria zenye ubaguzi wa kijinsia, ziwe za serikali au kimila.
- Kuikumbusha, kuielimisha na kuihamasisha jamii ya Tanzania itambue na kujua umuhimu wa kuwawezesha wanawake kushiriki katika michakato yote ya shughuli mbalimbali za maendeleo ili kuleta maendeleo chanya kwa wananchi katika sekta za kiuchumi na kijamii.
- Jukumu la kuwawezesha, kuwaendeleza, kuwashirikisha na kutowabagua wanawake wote bila kujali hali zao, uwezo walionao, jukumu hili ni la jamii nzima ya watanzania kuanzia ngazi ya Familia hadi Taifa na sio jukumu la serikali pekee au mashirika yasiyo ya kiserikali kama watu wengi wanavyodhani.
- Wanawake ni watu muhimu katika jamii, hivyo wanahitaji kupewa kipaumbele katika kuwawezesha kielimu, kijamii, kisiasa na kiuchumi, masuala yao yanahitaji kushughulikiwa kwa haraka kwa ujenzi wa Taifa lenye uhakika na mafanikio makubwa kupelekea Tanzania ya viwanda.

Ndugu Wananchi,

Napenda kutoa shukrani zangu za pekee kwa wadau wote ambao wametoa michango mbalimbali katika kuwawezesha wanawake katika Nyanja zote katika Wilaya yetu. Michango hiyo kwa wanawake na watoto wa kike ni pamoja na kuwapatia mikopo, elimu ya uundaji vikundi na ujasiriamali, huduma za afya msingi na elimu ya afya ya uzazi, elimu ya VVU/UKIMWI, kuwapatia elimu juu ya malezi bora na ustawi wa familia na jinsi ya kutambua unyanyasajia na ukatili wa kijinsia na jinsi ya kutolea taarifa na kuwafanya waweze kukuza uchumi wa viwanda wakiwa na ufahamu.

Ndugu Wananchi;

Familia zetu zisipokuwa imara kuwajibika ipasavyo kuwawezesha wanawake kiuchumi na kijamii zinaleta madhara mengi kwa wanawake ukizingatia wanawake ndiyo wazalishaji wakuu. Baadhi ya madhara hayo ni pamoja na:

- Idadi kubwa ya wanawake kukosa haki zao za msingi kama vile; elimu, huduma za afya, kuchagua/kuchaguliwa, kujieleza n.k
- Kuongezeka kwa unyanyapaa kwa wanawake na utelekezaji wa familia.
- Kuongezeka kwa idadi kubwa ya wanawake wanaoishi katika hali ya umasikini.
- Kupungua kwa ajira na kipato kwa wanawake

Matukio yote haya yanaenda kinyume na Sera ya Maendeleo ya wanawake ya (2000)

Hivyo ni jukumu letu sote kuweka mikakati ya kuhakikisha wanawake wote bila kujali hali zao wanapata haki zao zote za msingi zinazohitajika kwa ajili ya kuleta maendeleo chanya katika uchumi wa viwanda.

Ndugu Wananchi,

Napenda kutumia fursa hii kuipongeza Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kwa jitihada inazozifanya katika kuwawezesha wanawake kwa kufanya yafuatayo;

- Kutoa mafunzo mbalimbali kwa wanawake hususani elimu juu ya Ujasiriamali, uanzishaji wa viwanda vidogo vidogo, Jinsia na Maendeleo na malezi bora na ustawi wa familia, Unyanyasaji wa Kijinsia, VVU/UKIMWI,
- Kuhamasisha wanawake kushiriki katika kutoa maamuzi katika Nyanja mbalimbali za kijamii
- Kutoa mafunzo ya Sera ya wanawake, Sheria ya Mtoto, ulinzi na usalama wa mtoto masuala ya VVU/UKIMWI
- Kuwaunganisha wanawake na mashirika yasiyo ya kiserikali yanayotoa misaada au huduma mbalimbali kwa wanawake.

- Kuwapatia wanawake mikopo yenye riba na masharti nafuu kupitia mifuko ya maendeleo ya wanawake na vijana inayosimamiwa na Halmashauri ya Wilaya.

Hivyo natoa wito kwa jamii nzima ya wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kuunga mkono juhudi za serikali kusaidia upatikanaji wa haki za wanawake ili kuendelea kudumisha taifa linalojali amani na misingi ya haki za binadamu na hivyo kuboresha na kuinua uchumi wa wanawake..

Ndugu Wananchi,

Napenda kumalizia kwa kusema, jukumu la kuhakikisha kuwa wanawake wanakuwa katika uchumi wa viwanda na kuhakikisha wanapata haki zao za msingi ni la jamii nzima, hivyo kila mmoja wetu anatakiwa kutekeleza jukumu hilo kwa uhakika kwa lengo la kuhakikisha wanawake wanawezeshwa kushiriki katika michakato ya shughuli za maendeleo ili kuleta maendeleo chanya kwa wananchi katika sekta za kiuchumi na kijamii. Pia kudumisha amani na haki ya usawa kwa kila binadamu bila kujali tofauti zao. Jambo hili linawezekana iwapo kila mmoja wetu atawajibika kama kauli mbiu inavyosema.

“TANZANIA YA VIWANDA, WANAWAKE NI MSINGI WA MABADILIKO KIUCHUMI”

ASANTENI KWA KUNISIKILIZA